



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MM/MC/S.2/70 VOL I/118

Tarehe: 29/05/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anawatangazia waombaji wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kuleta maombi ya kazi kwa nafasi iliyoainishwa hapo chini, baada ya kupata idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa barua yenye Kumb. Na.FA.97/228/01"TEMP"/06 ya tarehe 06 Aprili, 2023 na kibali cha ajira mbadala kwa barua yenye Kumb.Na.FA.170/362/01"B"/76 ya tarehe 17/04/2023. Kutoka kwa Katibu Mkuu UTUMISHI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo basi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wataanzania wote wenye sifa ya kuomba nafasi ifuatayo:-

NAFASI YA DEREVA II (NAFASI 6).

1. Sifa za kitaaluma za mwombaji.

- a) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV).
- b) Awe na leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- c) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Draving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- d) Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi watafikiriwa kwanza.

2. Mshahara.

Ngazi ya mshahara TGS B

3. Majukumu ya Dereva II.

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na msimamizi wako wa kazi.

4. MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 na

4. MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wawasilishe picha mbili za hivi karibuni.
- iii. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- iv. Waombaji wote wawe hawajawahi kupatikana na kosa la jinai, kugushi vyeti au kufungwa jela.
- v. Waombaji waambatanishe nakala ya vyeti vya masomo na taaluma, Cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result slip" "statement of results" "Provisional results" au "Transcript". Maombi yake hayatapokelewa.
- vi. Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).
- vii. Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- viii. Waombaji waandike namba ya NIDA katika barua ya maombi au waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya vitambulisho (NIDA).
- ix. Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili.
- x. **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 11/06/2023 saa 9:30 Alasiri.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-


Mkurugenzi wa Manispaa,

S.L.P 92,

MTWARA-MIKINDANI.

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri
www.mtwaramikindanimc.go.tz.

Tangazo hili limetolewa na:-


Mangula Mayemba

KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA

MTWARA-MIKINDANI.

MKURUGENZI WA MANISPAA

MTWARA - MIKINDANI

S.L.P. 92

MTWARA